MKAKATI WA KUTEKELEZA KILIMO KWANZA MKOA WA DAR ES SALAAM. 2009

NGUZO YA 1 UTASHI WA KISIASA KUTOA MSUKUMO WA MAPINDUZI YA KILIMO					
	SHUGHULI	**MAJUKUMU**	**MKAKATI WA MKOA**	**MUDA WA UTEKELEZAJI**	**MTEKELEZAJI**
1.1	Kupitisha Dira ya KILIMO KWANZA	1 Kusisitiza utashi wa kisiasa katika ngazi zote za uongozi na nia thabiti kwa Watanzania kutekeleza Azimio la KILIMO KWANZA	i.Mkuu wa Mkoa na viongozi wa Chama ngazi ya Mkoa kuhamasisha jamii na kuwafanya wabadilishe mtazamo (mindset) ili watambue kuwa kilimo ni njia kuu ya uchumi na kuondoa umaskini kwa kufanya mikutano ya hadhara mijini na pembezoni mwa mji,kutumia vyombo vya habari ili kuhamasisha wananchi wawekeze katika kilimo. ii.Mkoa kufanya mikutano na wadau wa Kilimo ya kuelimisha juu ya mikakati ya kilimo kwanza. iii.Mkoakutenga fedha katika bajeti ya mwaka kwa ajili ya usimamizi, ufuatiliaji, tathmini na kutoa elimu ya Kilito,ufugaji na uvuvi katika Halmashauri na jamii kwa ujumla.	Muda Wote	Viongozi Wote
1.2	Kilimo cha wakulima wadogo, wa kati na wakubwa kiwe cha kisasa na cha kibiashara	2. Kuwaendeleza wakulima wadogo na wa kati kuwa wakulima wa kisasa na wa kibiashara.	**i.**Kufuatilia katika vituo vya utafiti ili kupata taaluma mpya zilizotokana na utafiti na kuzipeleka Halmashauri na hatimae kwa wakulima.(Research,Extension,farm	Muda Wote	Maafisa Kilimo Na Mifugo

			ers linkage). ii.Kufanya shughuli za uratibu na ushauri ili kuwezesha Halmashauri kushiriki katika maandalizi na maonesho ya Kilimo Nane nane Kanda ya mashariki. iii. Kuratibu shughuli za uratibu wa upatikanaji wa pembejeo na madawa ya mifugo na kufikisha katika kila Halmashauri zinazotakiwa. iv..Kufuatilia uanzishwaji wa vikundi vya wakulima,wafugaji na wasindikaji. v.Kuhakikisha kuwa Halmashauri zinaanzisha mashamba darasa ya mazao mbalimbali ili wakulima wajifunze kwa haraka kutokana na kuona. vi.Kufuatilia na kutoa ushauri ili kuwa na mashamba darasa yanayokidhi viwango vya kitaalam. vii.Kuhakikisha kuwa matoleo mapya ya kitaalam mfano mbegu mpya,madawa yanayowekwa katika mashamba darasa ili kuelimisha na kuwatangazia wakulima. viii.Kushiriki katika maonyesho na mikutano ya kutoa elimu kwa wakulima kwa kutumia mashamba darasa kwa ajili ya ushauri na uelimishaji (Back Stopping)		

			ix.Kuratibu ili kuwezesha Halmashauri kupata wanyama wadogo. x.Kuhakikisha wataalam wa ugani wanapangwa katika kila kata na mtaa.		
		2. Kuhimiza wakulima wa kati na wakubwa wachangie kwa ukamilifu kufanikisha KILIMO KWANZA	i.Kuhakikisha kuwa wakulima wanaelimishwa kulima mazao yanayoendana na hali ya hewa ya Mkoa (Agroecological zone) kwa mfano mihogo,viazi vitamu,mpunga,mtama,korosho,ma nanasi,mboga na matunda. ii.Kufuatilia na kuhakikisha kuwa wakulima wanahimizwa kununua na kutumia zana za kilimo mfano matrekta madogo (power tiller) na makubwa na matumizi ya wanyama kazi. iii. Kuhakikisha kuwa Halmashauri zinaweka katika mpango wa maendeleo bajeti ya kununua matrekta na kuyagawa kwa vikundi vya wakulima na kuyasimamia ili kuhakikisha kuwa yanatumika vizuri ili kuleta ufanisi katika kilimo. iv.Kufuatilia ili kuona elimu ya usindikaji na hifadhi bora ya mazao inafikishwa kwa wakulima. v.Kusimamia taratibu za soko la korosho ili kuhakikisha kuwa wasindikaji wanapata mazao toka kwa wakulima kwa ajili ya viwanda		

NGUZO YA 2
KUGHARAMIA KILIMO KWANZA

	SHUGHULI	MAJUKUMU	MKAKATI WA MKOA	MUDA WA UTEKELEZAJI	MTEKELEZAJI
2.1	Kuongeza Bajeti ya Serikali kwa ajili ya KILIMO KWANZA	1. Kutenga si chini ya asilimia 10 ya Bajeti ya Serikali kwa sekta ya kilimo kwa mwaka 2010/11 na kuendelea kuongeza kiwango hicho mwaka hadi mwaka kwa bajeti zinazofuata.	i.Kuhakikisha kuwa katika bajeti ya Mkoa fedha zinatengwa kwa ajili ya ufuatiliaji na uratibu wa shughuli za kilimo. ii.Kuhakikisha kuwa miradi endelevu inaibuliwa na kutekelezwa kwa ufanisi chini ya programu ya ASDP mipango ya maendeleo ya wilaya DADPS.	2010 Hadi 2015	Wakurugenzi Wa Halmashauri,Mkuu Wa Mkoa Na Wakuu Wa Wilaya
		2. Bajeti za wizara nyingine zote zizingatie utekelezaji wa KILIMO KWANZA	i.Wizara ya Ardhi kushirikiana na manispaa kugharamia kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ili kutenga ukanda wa kilimo (green belt) ii)Wizara ya viwanda Biashara na Masoko kutenga 10%ya bajeti ili kuboresha masoko ya jijini ili kupunguza uharibifu wa mazao ambayo ni kati ya 25% hadi 30% kwa mwaka.	2010 Hadi 2015	Wakurugenzi Wa Halmashauri Na Wakuu Wa Wilaya
		3. Kuwahimiza na kuwashawishi Washirika wetu wa	i.Kuhamasisha TASAF kuibua miradi mingi ya Kilimo hasa ya umwagiliaji.	Muda Wote	Mkuu Wa Mkoa, Wakurugenzi Wa Halmashauri

		maendeleo kusaidia KILIMO KWANZA	ii.Kuwasiliana na Taasisi ya Heifer International na CARITAS kuongeza kiwango cha ufadhili katika ufugaji wa ngombe na mbuzi wa maziwa.		
		4. Kuongeza Bajeti ya umwagiliaji kufikia hekta zisizo pungua milioni 7.	i.Kushirikiana na ofisi za umwagiliaji za kanda ili kupata fedha zaidi za kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika Manispaa za Ilala na Temeke. ii.Kushauri Halmashauri kuongeza bajeti ya DADPS katika miradi ya umwagiliaji ili kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka Hekta 140 hadi Hekta 10156 Kwa kuchimba visima virefu na vifupi,kuvuna maji ya mvua na kuongeza idadi ya pampu.	Kuanzia 2010/2011	Mkuu Wa Mkoa , Wakurugenzi wa Halmashauri Na Wakuu Wa Wilaya.
2.2	Kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).	Uanzishaji wa Benki ya Kilimo (TADB) uharakishwe ikiwa na mtaji wa kuanzia wa dola za Kimarekani millioni 500.	NA		
2.3	Kutafuta mtaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB)	1. Kuweka mipango ya upatikanaji wa mikopo na misaada kwa ajili ya Benki ya Kilimo kutoka vyanzo vya kimataifa.	NA		
		2. Kufanya mashauriano na benki za biashara na wadau wengine kumiliki dhamana za Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB)	NA		

2.4	Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB) kuwa na dirisha maalumu la mikopo ya kilimo (uzalishaji) itakayotolewa kwa masharti nafuu.	Kuongeza fedha kwenye Kitengo cha Kilimo cha Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB) kuwezesha kutoa mikopo ya muda mrefu na yenye masharti nafuu kwa misingi ya viwango vya kimataifa.	NA		
2.5	Mfuko Maalumu wa Fedha kwa ajili ya KILIMO KWANZA uanzishwe	Kutafuta mtaji wa kutosha kwa ajili ya Mfuko Maalumu wa Fedha kugharimia upimaji ardhi, uwekezaji, ujengaji uwezo wa wafanyakazi na dhamana ya upatikanaji wa mikopo kukidhi mahitaji ya KILIMO KWANZA	NA		
2.6	Kuimarisha Mfuko wa Programu ya Mkakati wa Maendeleo ya Kilimo (ASDP) kutekeleza KILIMO KWANZA.	Kupanua ushiriki wa Washirika wetu wa Maendeleo katika Mfuko wa Programu ya Mkakati wa Maendeleo ya Kilimo (ASDP)	NA		
2.7	Kuhamasisha sekta binafsi iongeze uwekezaji katika sekta ya Kilimo kuanzia ngazi ya chini, kati na wakubwa.	Kuhamasisha sekta binafsi kuongeza uwekezaji katika utekelezaji wa KILIMO KWANZA.	i.Kuhakikisha kuwa sheria ndogo za kilimo zinatumika ili kuhakikisha wenye mashamba yao wanayasafisha na kuyaendeleza kwa kilimo. ii.Kusisitiza uundwaji wa kamati za kilimo za mtaa ambazo zitasimamia matumizi ya ardhi. iii.Kuhamasisha makampuni yenye viwanda hapa jijini kuanzisha viwanda vya kusindika mazao ya kilimo kama mboga na matunda.	Muda Wote	Mkuu Wa Mkoa,Wakurugenzi Wa Halmashauri Na Wakuu Wa Wilaya.

			iv.Kushirikisha Taasisi na makampuni yanayosindika mazao ya kilimo kutoa elimu kwa wananchi/jamii jinsi ya kutumia teknologia ya kisasa katika usindikaji wa mazao ya kilimo kwa mfano ukamuaji wa mbegu za mafuta,mfano chikichi,nazi na ubanguaji korosho,usindikaji wa mhogo, mtama ,soya,kutengeneza mvinyo wa rosella,ndizi,mananasi ,mapapai nk Kusindika matunda na mboga kupata juisi,achali,jamu kwa ajili ya soko la ndani na nje. v.Kuhamasisha makampuni mbalimbali yanayozalisha zana za kilimo kama SIDO,Nyumbu,IPI,CAMATEC,MZINGA CORPORATION,INTERMEC Kubuni aina mbalimbali za mashine za kusindika mazao mbalimbali hasa mboga na matunda.		
2.8	Kuviwezesha Vyama vya Ushirika na SACCOS viweze kutafuta, kusimamia na kuelekeza mitaji kwa wanachama wao ili kuimarisha uzalishaji katika kilimo.	1. Kuandaa mkakati wa taifa wa kuongeza uelewa wa maswala ya fedha.	NA		
		2. Kuimarisha uwezo wa Vyama vya Ushirika vya Wakulima na SACCOS kusimamia ipasavyo rasilimali katika utekelezaji wa KILIMO KWANZA.	i.Kuboresha chama cha ushirika cha mkoa DARECU ili kiweze kupata mkopo kwa ajili ya kununua korosho na kusambaza madawa ya ruzuku za korosho katika vyama vya ushirika vya msingi. ii.Kuhamasisha vyama vya ushirika vya msingi 23 vilivyopo viweze	2009 Hadi 2015	Mkuu Wa Mkoa,Wakurugenzi Wa Halmashauri, KILIMO.

			kuanzisha vyama vya akiba na mikopo SACCOS Ili kuweza kupata mikopo na kukopesha wakulima kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo na zana za kilimo. iii.Mkoa uhamasishe vyama vya ushirika vya msingi katika kutoa elimu ya kilimo bora cha Korosho ili waweze kupata korosho bora.		
2.9	Kuandaa utaratibu wa kisheria wa kuyawezesha Mabenki ya Biashara kukopesha asilimia ya amana zao kwa ajili ya kilimo kwa masharti nafuu.	1. Kujadiliana na mabenki ya biashara na wadau wengine kuhusu kukopesha sekta ya kilimo kwa masharti nafuu.	NA		
		2. Kurekebisha kanuni na taratibu za kurahisisha utoaji mikopo ya uzalishaji katika Kilimo.	NA		
		3. Kuhimiza na kusaidia Mabenki kuwa wabunifu wa utoaji mikopo inayolenga utekelezaji wa KILIMO KWANZA.	NA		
2.10	Kuimarisha uanzishaji wa Mabenki ya Wananchi katika mikoa yote ya Tanzania.	1. Kuanzisha mabenki ya wananchi na asasi za fedha katika maeneo ya vijijini na wilayani.	i.Kuhamasisha Benki ya Wananchi wa Dar es Salaam (DCB)kuwa na matawi pembezoni mwa mji au kuwa na mobile Bank.	Kuanzia 2010	Mkuu Wa Mkoa Wakurugenzi wa Halmashauri Za Manispaa,KILIMO Na TAMISEMI.
		2. Kujenga uwezo wa usimamizi wa Mabenki ya Wananchi na kuimarisha chama chao.	ii.Kuhamasisha wananchi kujiunga katika vikundi na kuanzisha vyama vya ushirika vya akiba na mikopo (SACCOS). iii.Kuhamasisha vyama va ushirika vya msingi vya mazao ambavyo ni 23 kuanzisha SACCOS.Hadi sasa Mkoa una SACCOS mbili za mazao		

			ambazo ni Msongola SACCOS na Vumilia Ukooni SACCOS. iv.Kuhamasisha Benki zilizopo hapa jijini kutoa mikopo kwa SACCOS ili kutoa mikopo kwa Wakulima/Wafugaji.		
2.11	Kuanzisha vitengo maalum katika asasi za fedha kwa ajili ya kutoa mikopo ya kilimo	Benki za Wananchi na asasi nyingine za fedha kama vile Benki ya Posta Tanzania (TPB), AZISE na taasisi za fedha kwa wateja wadogo zianzishe vitengo maalum kwa ajili ya kutoa mikopo ya kilimo.	NA		
2.12	Kuanzisha masoko ya mazao (Commodity Exchanges) na uwezeshaji wa makampuni ya kilimo yaweze kuuza hisa zao kwenye Soko la Mitaji la Dar es Salaam.	1. Kuanzisha Masoko ya Mazao (Commodity Exchanges)	NA		
		2. Kuwezesha uuzaji wa hisa za makampuni ya kilimo katika Soko la Mitaji la Dar es Salaam.			
2.13	Mifuko ya Pensheni, Uwezeshaji na mifuko mingine ikubaliane utaratibu wa kuwekeza asilimia ya pato lao katika uzalishaji wa sekta ya kilimo kwa masharti nafuu.	1. Kujadiliana na mifuko ya pensheni na mifuko mingine ya uwezeshaji kukopesha kwa masharti nafuu kwa ajili ya uzalishaji wa sekta ya kilimo.	NA		
		2. Kuanzisha Mfuko wa Dira Tanzania (Vision Tanzania Fund) kwa ajili ya kukopesha sekta ya kilimo (uzalishaji).	NA		
2.14	Kuanzisha utaratibu wa malipo ya ustawi wa jamii (Social Security) kwa wakulima	1. Kuanzisha mfuko maalum wa malipo ya ustawi wa jamii kwa wakulima	NA		
		2. Kuhamasisha wakulima wajiunge na mifuko ya ustawi wa jamii.			

2.15	Kuandaa sera na taratibu kwa ajili ya makampuni ya bima kutoa kinga ya bima na mikopo ya uzalishaji ya sekta ya Kilimo.	Kujadiliana na makampuni ya bima ili yaanzishe bima ya kinga na mikopo ya uzalishaji katika sekta ya kilimo.	NA		

NGUZO YA 3
MUUNDO MPYA WA TAASISI KWA AJILI YA USIMAMIZI WA KILIMO KWANZA
UBORESHAJI WA MFUMO WA UTAWALA WA KILIMO

	SHUGHULI	MAJUKUMU	MKAKATI WA MKOA	MUDA WA UTEKELEZAJI	MTEKELEZAJI
3.1	Kurekebisha muundo wa kitaasisi kwa ajili ya utekelezaji wa KILIMO KWANZA	1. Kusisitiza utawala bora katika sekta zote za uchumi na katika ngazi zote. 2. Kuimarisha Wizara ya Kilimo na kuboresha kazi za kongano ya kilimo.	NA		
		3. Kuingiza masuala ya mazingira katika shughuli za KILIMO KWANZA	i.Kuwaelimisha wakulima/wafugaji umuhimu wa kutunza mazingira ili kulinda mabadiliko ya tabia nchi ili kupunguza athari za kiafya kwa walaji na kuzuia uchafuzi wa maji kwa kutumia viwango na aina sahihi za pembejeo. ii.Kusimamia sheria ndogo ya jiji la Dar es Salaam inayosisitiza ufugaji wa ndani (zero grazing) badala ya kuchunga mifugo. iii.Kuzingatia kilimo cha mchanganyiko wa mazao na mazao miti(Agroforest) na kuhakikisha kuwa kila Halmashauri inabustani ya miche bora ya miti na matunda. iv.Kusimamia sheria ya mazingira ambayo inasisitiza kilimo kisizidi kiwango cha mita 60 kutoka vyanzo	Muda Wote	Ofisi Ya Makamu Wa Rais ,Mkuu Wa Mkoa, Wakurugenzi Wa Halmashauri, Wataalam Wa Kilimo Na Mifugo

			vya maji. v.Kuelimisha jamii kutumia teknologia ya makinga maji kwenye miinuko mikali. vi.Kuelimisha wakulima kutumia kilimo cha mzunguko wa mazao. v.Kuzuia shughuli za Kilimo kwenye miinuko mikali sana.		
		4. Kuanzisha Wakala wa Taifa wa Umwagiliaji (National Irrigation Agency - NIA) unaojitegemea chini ya Wizara ya Kilimo. 5. Kuunganisha mifuko miwili ya umwagiliaji ch ini ya Wakala wa Taifa wa Umwagiliaji (NIA).	NA		
3.2	Kuanzisha utaratibu wa kuratibu uhusiano na wizara nyingine zinazohusiana na maswala ya kilimo.	Kuanzisha Kamati ya Kilimo ya Baraza la Mawaziri kuratibu shughuli za wizara zote zinazohusiana na kilimo.	NA		
3.3	Kuanzisha utaratibu wa ubia wa sekta ya Umma na ya Binafsi kwa ajili ya KILIMO KWANZA	1. Kuanzisha Tume ya Taifa ya Kilimo na Vyama vya Ushirika (National Agriculture and Cooperatives Commission - NACC) kwa ajili ya ubia wa sekta ya Umma na ya Binafsi katika kuendeleza kilimo pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa KILIMO KWANZA.	NA		

		2. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa KILIMO KWANZA	i.Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikakati katika ngazi zote iwe kwa muda muafaka. ii.kuhakikisha kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya kilimo zinafikia walengwa na kutumika kulingana na lengo lililowekwa. iii.Kuweka lengo la uzalishaji mazao na kupima utekelezaji kila robo mwaka. iv.Kuhakikisha kuwa wataalam wa ugani wako katika maeneo yote ya kilimo /ufugaji. v.Kufanya vikao kila robo mwaka ili kupima mafanikio na kujadili changamoto zilizojitokeza.	Kila robo ya mwaka.	Maafisa Kilimo Mifugo wa Mkoa na wilaya.
3.4	Kuimarisha Vyama vya Wakulima kwa ajili ya kuboresha ushirikiano na Serikali katika utungaji wa sera, mikakati, utekelezaji na tathmini ya utendaji kazi wa sekta ya kilimo.	Kusaidia kujenga uwezo wa wakulima na Vyama vya Wakulima katika utekelezaji wa programu za KILIMO KWANZA	i.Kuhakikisha kuwa teknologia mpya za uzalishaji kutoka kwa watafiti zinafikia wakulima. ii.kuhakikisha kuwa pembejeo za kilimo na madawa ya mifugo yanapatikana kwa bei za ruzuku. iii.Kuhakikisha kuwa Halmashauri zinapiga marufuku mtindo wa madalali kuuza mazao kwenye masoko.	Muda Wote	Wakurugenzi Wa Halmashauri Wataalam Wa Kilimo Na Mifugo

			iv Kuwashawishi wakulima kujiunga katika vikundi ili waweze kuuza mazao kwa urahisi katika masoko na kutatua matatizo mengine katika kilimo.		

NGUZO YA 4 MABADILIKO YA MFUMO WA KIMKAKATI WA KILIMO KWANZA					
	SHUGHULI	**MAJUKUMU**	**MKAKATI WA MKOA**	**MUDA WA UTEKELEZAJI**	**MTEKELEZAJI**
4.1	Kubainisha maeneo ya kipaumbele kwa ajili ya vyakula muhimu ili nchi ijitosheleze kwa chakula	1. Kuandaa mipango ya uzalishaji wa mazao ya chakula muhimu kama vile mahindi, mihogo, mpunga, jamii ya maharage, samaki, nyama na bidhaa za maziwa, ngano, ndizi, viazi mviringo, ulezi na mtama.	i.Kuhimiza Kilimo cha mazao yanayoendana na Hali ya hewa ya Dar es Salaam na kuhamasisha wakulima kutumia mbegu bora.mfano wakulima watumie,mbegu za mihogo,viazi kunde na mbaazi ambazo zinahimili ukame, magonjwa na wadudu ii.Kuhimiza ufugaji wa wanyama wadogo kama kuku,njiwa,sungura,simbilisi na bata.Pia mkoa unahimiza ufugaji samaki katika mabwawa.	Muda Wote	IWataalam Wa Kilimo Na Mifugo
		2. Kuanzisha utaratibu wa kuchanganya mihogo katika usagishaji wa mahindi na ngano.	i.Kuhakikisha wakulima wanawezeshwa kupitia mpango wa maendeleo ya DADPS kupatiwa mashine za kusindika mhogo.	Kuanzia 2010/2011	Viwanda; TAMISEMI; Wakurugenzi Wa Halmashauri
4.2	Kubainisha maeneo ya kipaumbele ya uzalishaji wa mazao yanayoweza kuboresha kilimo haraka kwa kutumia gharama na utaalam mdogo na kukidhi mahitaji ya soko la ndani/nje na kuongeza	Kuweka na kutekeleza mipango ya kugharamia uzalishaji wa pamba, alizeti, katamu, ufuta na mawese.	. NA		

	ajira.				
4.3	Kubainisha maeneo ya kipaumbele na uzalishaji wa mazao ya kilimo cha bustani (horticulture)	Kuweka mipango ya uzalishaji mazao kama vitunguu, embe, zabibu, maparachichi, mananasi, ndizi, nyanya mboga na viungo.	i.Kuhamasisha na kutoa elimu kwa wakulima kulima mazao yenye tija hasa matunda (embe, nanasi, makakara, matikiti, machungwa, maparachichi, mapapai mapera, mafenesi)na mboga (mboga za majani, matango, nyanya, bamia, bilinganya, nyanya chungu, paprika, pilpili kali, hoho na vitunguu) na kilimo cha maua. ii.Kuhakikisha Kila Halmashauri inakuwa na bustani za kuzalisha miche bora ya matunda iliyobebeshwa (grafted) ambayo inachukua muda mfupi kukomaa na kusambazwa kwa wakulima kwa gharama kidogo	Muda Wote	Wakurugenzi Wa Halmashauri
4.4	Kubainisha maeneo ya kipaumbele ya uzalishaji mazao yenye ongezeko kubwa la thamani kama vile nyuzi, mimea ya nishati n.k.	Kuweka mipango kwa ajili ya uzalishaji wa mkonge, miwa, mtama mtamu na mbegu za mafuta kwa ajili ya nishati na bidhaa nyingine zilizoongezwa thamani.	i.Kuhamasisha wakulima kulima kilimo cha Alizeti,michikichi,Ufuta na Karanga.	Kuanzia Msimu Wa 2009/2010	Wakuu Wa Wilaya,Wataalamu Wa Kilimo Na Mifugo.

4.5	Kuanzisha Kamati ya Ushauri kuhusu Mabadiliko ya Mfumo wa Kilimo.	Kuunda Kamati ya Ushauri inayojumuisha Sekta Binafsi kushauri maeneo ambayo shughuli mbalimbali katika Mabadiliko ya Mfumo wa Kilimo zitafanywa.	i.Kuanzisha /Kuunda kamati za kuendeleza Kilimo za Mkoa ,Wilaya,Kata na mitaa zitakazojumuisha wadau kutoka serikalini na sekta binafsi.	Kuanzia 2010/2011	TAMISEMi; Mkuu Wa Mkoa Wakurugenzi Wa Halmashauri NGOS
4.6	Kufanya uchambuzi wa mlolongo wa mazao yaliyopewa kipaumbele	Kufanya uchambuzi wa mlolongo wa mazao yaliyopewa kipaumbele kwa kuangalia maeneo nyeti pamoja na jinsi ya kuwaunganisha na kuwashirikisha wazalishaji wa mazao ya kilimo na wasindikaji.	i.Kuhamasisha wafugaji kuunda vikundi ili kusindika maziwa ii.Kuhamasisha usindikaji wa mihogo, mboga na matunda. iii.Kuhimiza usindikaji wa zao la ngozi iv.Kuhamasisha uzalishaji na usindikaji korosho v.Kuhamasisha watu wenye uwezo Kujenga machinjio ya kisasa kwa ajili ya kuchinja na kusindika nyama.	Kuanzia Sasa	TAMISEMI; Mkuu Wa Mkoa Wakurugenzi Wa Halmashauri
4.7	Kutunga sheria ya kuboresha Mfumo wa Kilimo cha Mkataba (Contract Farming System - CFS)	1. Kuharakisha utungaji wa Sheria ya Mfumo wa Kilimo cha mkataba. 2. Kuweka misingi ya kujenga uwezo wa wadau wanaojihusisha na Kilimo kwa Mkataba (CFS)	NA		

NGUZO YA 5 UPATIKANAJI WA ARDHI KWA AJILI YA KILIMO KWANZA					
	SHUGHULI	**MAJUKUMU**	**MKAKATI WA MKOA**	**MUDA WA UTEKELEZAJI**	**MTEKELEZAJI**
5.1	Kurekebisha Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya 1999.	1. Kurekebisha Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya 1999 ili kuwezesha upatikanaji wa ardhi kwa uwekezaji wa KILIMO KWANZA.	NA		
		2. Kuimarisha uwezo wa Maafisa Ardhi wa Wilaya na Halmashauri za Wilaya kutekeleza majukumu yao yanayohusu ardhi.			
5.2	Kuharakisha mfumo wa upatikanaji ardhi	1. Kuhimiza utekelezaji wa sheria kuhusu mipango ya matumizi ya ardhi vijijini na mipango miji kufanya michakato itakayojumuisha utoaji wa hati miliki.			
		2. Kutenga ardhi kwa ajili ya mazao na mifugo na kutangaza maeneo hayo katika Gazeti la Serikali.	i.Mkoa utahakikisha kuwa Kila Halmashauri ya Manispaa inaainisha maeneo ya ukanda wa kijani (green belt) ambayo yatalindwa kisheria kwa ajili ya shughuli za kilimo na yamilikishwe kisheria.	2010 Hadi 2015	Wakurugenzi Wa Halmashauri,Mkuu Wa Mkoa,Wakuu Wa Wilaya

		3. Kutenga rasilimali za kutosha kwa Halmashauri za Wilaya/Miji ziweze kutekeleza shughuli zilizopangwa kuhusiana na ardhi.	NA		
		4. Kujenga uwezo wa Ofisi za Ardhi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili zisimamie ipasavyo masuala ya ardhi na kuimarisha usimamizi wa Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya.			
		5. Kupitia upya gharama za upimaji wa ardhi kwa ajili ya utoaji wa Hati za Usajili.	NA		

5.3	Kuharakisha utatuzi wa migogoro ya ardhi.	1. Kuanzisha mifumo ya uharakishaji wa utatuzi wa migogoro ya ardhi.	NA		
		2. Kutenga fedha kwa ajili ya kuharakisha hukumu katika mfumo wa Mahakama (kugharamia watumishi).			
		3. Kuanzisha Mabaraza ya Ardhi ya Kata na Vijiji na kuimarisha yaliyopo ili yajihusishe na utatuzi wa migogoro ya ardhi.			
5.4	Kuboresha muundo katika usimamizi wa ardhi	Kupitia na kuboresha utaratibu uliopo wa kugawa ardhi	NA		
5.5	Kuingiza maeneo yanayofaa kwa kilimo katika mipango ya maendeleo ya miji.	Mipango ya maendeleo ya miji kutambua na kujumuisha maeneo ya kilimo.	i.Kuhakikisha kuwa katika upangaji wa miji kuna maeneo yanayotengwa kwa ajili ya kilimo na kuhifadhi ardhi	Kuanzia 2009	Mkuu Wa Mkoa, Wakurugenzi Wa Halmashauri, Wakuu Wa Wilaya.

5.6	Kutenga ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo (Land Bank)	1. Wakuu wa Mikoa kutenga maeneo maalum ya ardhi (Land Bank) kwa ajili ya uwekezaji, uzalishaji na biashara.	i.Serikali kuangalia uwezekano wa kuongeza maeneo ya Mkuranga,Kisarawe na Bagamoyo ili kupata eneo zaidi la kilimo	2010 Hadi 2015	TAMISEMI Wakuu Wa Mikoa, Ardhi; Kilimo;
		2. Kubainisha na kuweka kumbukumbu za ardhi isiyotumika vizuri kwa ajili ya uwekezaji wa Kilimo.	NA		
		3. Kuandaa hatua na taratibu za kisheria zitakazoviwezesha vijiji na wanakijiji kutumia ardhi kama hisa kwa shughuli za ubia na wawekezaji.			
		4. Kupitia upya haki miliki za Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ili kuwezesha Watanzania kuingia ubia katika uwekezaji unaohusu ardhi.	NA		
		5. Kuandaa mfumo wa kutathmini ardhi utakao onyesha thamani yake halisi kwa madhumuni ya uwekezaji.	NA		
		6. Kuhimiza matumizi ya sheria ili kujiepusha na kuhodhi na ulanguzi wa ardhi.	NA		

5.7	Kutumia kwa ukamilifu ardhi ambayo hivi sasa inamilikiwa na Serikali na Taasisi za Serikali.	Kutumia kikamilifu ardhi ambayo inamilikiwa na Serikali na Taasisi za Serikali kwa ajili ya uzalishaji wa kilimo.	i.Kuainisha maeneo yanayofaa kwa kilimo na kupendekeza mazao yanayofaa kwenye maeneo hayo na kuwaazima wananchi kwa ajili ya kuendeleza shughuli za kilimo. Mfano Luguruni shamba la mifugo,chamazi Muhimbili rehabilitation,Mloganzila na Kisopwa,JKT Kimbiji.Hatua hii ni kuondoa wanyama waharibifu wa mazao.	Kuanzia 2009	Mkuu wa Mkoa, Wakurugenzi Wa Halmashauri, Wataalam Wa Kilimo Na Mifugo.

NGUZO YA 6 VIVUTIO VYA KUCHOCHEA UWEKEZAJI KATIKA KILIMO.					
	SHUGHULI	**MAJUKUMU**	**MKAKATI WA MKOA**	**MUDA WA UTEKELEZAJI**	**MTEKELEZAJI**
6.1	Kuainisha vivutio vya sera ya kodi na vivutio vingine ili kuchochea maendeleo ya KILIMO KWANZA.	Kuanzisha Kamati Maalum kupitia na kupendekeza vivutio muhimu, ikiwa ni pamoja na sera ya kodi na vivutio vingine ili kuchochea maendeleo ya KILIMO KWANZA	NA		
6.2	Kubuni na kutekeleza hatua za kuimarisha ushindani wa kilimo cha Tanzania.	Kupitia gharama za kufanya biashara katika sekta ya kilimo ili kuiwezesha kuwa ya ushindani zaidi.	. NA		
6.3	Kuondoa vikwazo vya masoko kwa mazao ya kilimo	1. Kuongeza mtaji kuwezesha Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa kusimamia bei za mazao ya chakula na kuifanya Serikali iwe mnunuzi mkuu wa kutegemewa na kwa bei za soko huria.	NA		
		2. Kuongeza uwezo wa Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (NFRA) kununua mazao kwa kiwango kikubwa na kukihifadhi.			
		3. Kuhamasisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika ununuzi na uhifadhi wa mazao ya chakula.	NA		

		4. Kuhifadhi akiba ya chakula cha miezi 6 hadi mwaka 1 ili kuhakikisha akiba ya chakula na mwenendo wa bei ni wa kuridhisha. 5. Kuondoa vikwazo vya mipaka kwa mauzo ya mazao ya chakula.	NA		
6.4	Utumiaji wa vipimo na viwango halali katika biashara uimarishwe.	1. Taratibu na sheria za kuuza mazao kwa uzito na vipimo vinavyotakiwa zizingatiwe; (Kutotumia lumbesa, pakacha au sado, n.k.) 2. Vyombo vya sheria kutekeleza taratibu na kanuni za uwekaji madaraja (grading) na ufungashaji (packaging) wa bidhaa za kilimo.	NA		
6.5	Kuanzisha chombo cha kuendeleza mazao mchanganyiko.	Kuanzisha chombo cha kuendeleza na kusimamia uzalishaji na masoko ya mazao ya mchanganyiko.	NA		
6.6	Kuboresha bei za mazao	Kuanzisha utaratibu wa kuboresha bei za bidhaa za kilimo	i.Kuhimiza na kuazisha masoko ya mazao katika maeneo karibu na Wakulima ili kupunguza nguvu ya walanguzi. ii.Kusisitiza matumizi ya vipimo vinavyojulikana kimataifa	Kuanzia 2009	Wakurugenzi Wa Halmashauri, Mkuu Wa Mkoa, Wakuu Wa Wilaya

NGUZO YA 7
UENDELEZAJI WA VIWANDA KATIKA KULETA MAPINDUZI YA KILIMO.

	SHUGHULI	MAJUKUMU	MKAKATI WA MKOA	MUDA WA UTEKELEZAJI	MTEKELEZAJI
7.1	Viwanda kwa ajili ya kushughulikia mahitaji ya wazalishaji wa kilimo.	Kubainisha na kushughulikia mahitaji ya wazalishaji wa kilimo wa Tanzania.	i.Kuhakikisha kuwa Kila Halmashauri inaainisha mahitaji ya zana,pembejeo na madawa kuendana na malengo ya uzalishaji na mahitaji ya wakulima na kuyawasilisha wizara ya Kilimo chakula na Ushirika ili yashughulikiwe.	Kila Robo Ya Mwaka.	KILIMO, Wakurugenzi Wa Halmashauri
7.2 7.2.1	<u>Nyenzo za Uzalishaji wa Kilimo (Backward Linkages)</u> Kuongeza uzalishaji na matumizi ya mbolea.	1. Kuongeza na kuboresha uzalishaji na ubora wa mbolea za kemikali kutoka uzalishaji wa sasa wa Phosphate na NPK unaofanyika Minjingu hadi kufikia tani 300,000 na zaidi kwa mwaka ifikapo mwaka 2010. 2. Kutafiti uzalishaji wa mbolea za kemikali zinazotumia Nitrogen kwa kutumia gesi ya asilia inayopatikana nchini.	NA		

		3. Kuongeza huduma za ugani ili kupanua mahitaji na kuhakikisha matumizi sahihi ya mbolea.	i. Kuwapanga wataalam wa ugani 155 katika maeneo pembezoni mwa mji ambapo mazao ya kilimo na ufugaji unafanyika. ii. Kuhakikisha kuwa wataalam wanapatiwa vitendea kazi,magari 3,pikipiki 49,baiskeli 101,extension kits 306,video camera3 na digital camera 3. iii. Kuhakikisha kuwa kila Halmashauri inafundisha vijana 10 kutoka vikundi vya uzalishaji vya vijana kujifunza shughuli za uzalishaji. iv.Kujenga nyumba 9 za wataalam wa Kilimo na Mifugo v.Kuhakikisha kila Afisa Ugani anakuwa na shamba darasa na shamba la mfano na mfugaji wa mfano. vi.Kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa wataalam wa ugani vii.Kuhamasisha watu wenye uwezo vijijini kuanzisha maduka ya pembejeo za kilimo na dawa za mifugo viii.Kuhamasisha vyama vya Ushirika vya Msingi,kuanzisha vyama vya akiba na mikopo SACCOS ili kuweza kukopesha wakulima kwaweze kununua pembejeo.	Kuanzia 2010 hadi 2015	KILIMO,TAMISEMI Wakurugenzi Wa Halmashauri Na Wataalamwa Kilimo/Mifugo
		4. Kuwezesha upatikanaji wa mbolea ya kutosha.	NA		

7.2.2	Kuboresha uzalishaji wa mbegu.	1. Kufanya tathmini ya utendaji wa kampuni zote za mbegu zilizobinafsishwa (TANSEED) ili kukidhi mahitaji ya taifa	NA		
		2. Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mbegu ili kukabili matumizi yaliyoshamiri ya mbegu zisizo halisi.			
		3. Kutoa ruzuku inayohusu mbegu bora na zilizoidhinishwa kwa wakulima wadogo.	NA		
		4. Kuwezesha na kuimarisha Taasisi ya Uidhinishaji Mbegu Rasmi Tanzania (Tanzania Official Seed Certification Institute - TOSCI) kuwa mdhibiti.	NA		
		5. Kutoa hataza kwa matokeo ya utafiti wa mbegu ili kulinda aina za mbegu zinazozalishwa nchini	NA		
7.2.3	Kuainisha na kuimarisha uwezo unaohitajika kwa kuendeleza sekta ya mifugo.	1. Kuimarisha Kituo cha Taifa cha Utovishaji (National Artificial Insemination Centre - NAIC) kilichoko Arusha na kuanzisha vituo vya kuhifadhi na kusambaza mbegu za madume katika mikoa yote.	NA		
		2. Kufufua na kuanzisha vituo vya uzalishaji mifugo na mitamba.			

		3. Kuhakikisha uzalishaji wa kutosha wa dawa na vyakula vya mifugo hapa nchini.			
		4. Kukarabati viwanda vyote vya maziwa vilivyopo nchini na kuanzisha vituo vya kukusanyia maziwa.			
7.2.4	Kuainisha na kuimarisha uwezo unaohitajika kwa kuendeleza sekta ya uvuvi	1. Kuwekeza katika nyenzo zitakazowezesha matumizi kamilifu ya rasilimali za majini.			
		2. Kutayarisha na kuwezesha programu ya ufugaji wa samaki kwa kila wilaya.	Kuhakikisha Kila Halmashauri kupitia mradi wa DADPS inatenga fedha kwa vikundi vya wakulima ili kujenga mabwawa.	2010 Hado 2015	Wakurugenzi Wa Halmashauri Za Manispaa
		3. Kuimarisha na kupanua vituo vya uzalishaji samaki kwa ajili ya kusambaza vifaranga wa samaki.			
		4. Kuhimiza hatua na taratibu za uhifadhi wa ufugaji wa samaki na kulinda mazingira.	i.Kamati iliyoundwa na Halmashauri zote tatu,iwezeshwe na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na uvuvi kupatiwa boti kwa ajili ya kufanya patrol na usafiri kwa ajili ya kubebea makokoro yanayokamatwa. ii.Kuhakikisha kuwa doria inafanyika kuhakikisha kuwa uvuvi haramu unathibitiwa.	Muda Wote	Wakurugenzi Wa Halmashauri Za Manispaa
7.2.5	Kuongeza uzalishaji wa dawa za kilimo nchini.	1. Kuanzisha viwanda vya uzalishaji wa dawa za kilimo nchini.	NA		
		2. Kuhimiza usimamizi na uangamizaji wa wadudu na	Kuwafundisha wakulima mbinu mbalimbali za kudhibiti wadudu	Muda Wote	Wataalam Wa Kilimo.

		wanyama waharibifu.	na wanyama waharibifu kama kutumia wanyama waharibifu kama kitoweo mfano nguruwe pori na ndege,kupanda mimea inayofukuza wadudu kama marigold na matumizi sahihi ya dawa za kuangamiza wadudu.		
		3. Kuelimisha wakulima kuhusu masharti na matumizi sahihi ya dawa za kilimo.	i.kuhakikisha kuwa Wataalam wa ugani wanapata mafunzo ya matumizi sahihi na salama ili watoe mafunzo kwa wakulima.	2010 Hadi 2015	Wakurugenzi Wa Halmashauri
7.2.6	Uzalishaji wa zana na vifaa vya kilimo	1. Viwanda vya zana za kilimo vilivyo binafsishwa vizalishe vifaa vya kilimo.	NA		
		2. Kuanzisha uzalishaji wa mashine, vifaa na zana za kilimo nchini			
		3. Kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vya sekta ya kilimo katika ngazi ya Afrika Mashariki.	NA		
7.3 7.3.1	<u>Utunzaji, Usindikaji na Uuzaji wa mazao ya kilimo</u> <u>(Forward linkages):</u> Upanuzi wa viwanda vya kuchakata na kusindika mazao ya kilimo.	1. Kuimarisha sera na taratibu za kukataza usafirishaji mazao ghafi nchi za nje na kuongeza ushuru kwa bidhaa shindani zinazoagizwa toka nchi za nje na kufanya tathmini ya mara kwa mara.	NA		
		2. Kutunga sheria kali ili kuzuia bidhaa za kilimo zilizosindikwa au kuchakatwa kwa kiwango cha chini kuletwa nchini.	NA		

		3. Kuendesha kampeni ya "Nunua Bidhaa za Tanzania" kuanzia na manunuzi ya Serikali.			
		4. Kurudisha umiliki na kufufua viwanda vya kusindika au kuchakata mazao ya Kilimo vilivyo binafsishwa ambavyo havijafanya kazi mpaka sasa (viwanda vya korosho, ngozi, nguo n.k.)	NA		
		5. Kuwasaidia na kuwaunga mkono wasindikaji na wachakataji mazao ya kilimo kwa kuwapa vivutio na misaada mingine.			
		6. Kuisaidia SIDO kupanua usindikaji na uchakataji mazao ya kilimo.			
		7. Kuanzisha viwanda vya ufungashaji vya kiwango cha juu kukidhi ongezeko la mazao ya kilimo yaliyosindikwa na yaliyochakatwa.			

7.3.2	Usimamizi wa kupunguza upotevu na uharibifu wa mazao baada ya kuvuna.	1. Kuanzisha maghala ya kuhifadhia mazao wilayani.	1.Kusisitiza ukarabati wa maghala ya mazao yaliyopo na pale ambapo hamna kujenga mapya katika kata zenye zao la korosho.	Kuanzia 2010 hadi 2011	TAMISEMI; KILIMO Wakurugenzi wa Halmashauri
		2. Kuhimiza uwekezaji wa sekta binafsi katika vifaa vya kuhifadhia mazao yanayoharibika upesi na mazao mengine.	NA		

		3. Kuandaa mkakati wa kuelimisha wakulima njia bora za kuhifadhi na usimamizi wa mazao ya kilimo.	i.Kuhakikisha kuwa Halmashauri zinatoa elimu kwa wakulima /wafugaji juu ya uhifadhi wa mazao kama mboga ,matunda,maziwa,nyama,samaki na ngozi ii.Kuhimiza wakulima /wafugaji kujiunga katika vikundi ili waweze kupata mikopo ya kununulia vifaa vya kuhifadhia mazao.	Kuanzia 2009	Maafisa Kilimo, Mifugo Na Maafisa Ushirika.
		4. Kuhimiza uwekezaji katika urutubishaji chakula ili kuboresha lishe.	NA		
7.3.3	Kuimarisha mkakati wa biashara na usimamizi wake	1. Kuanzisha vituo vya taarifa za masoko kuwawezesha wakulima kuelewa hali ya biashara katika masoko mbalimbali.	NA		
		2. Kuboresha mfumo wa usambazaji wa pembejeo za kilimo ili kufikisha kwa wakulima kwa wakati muafaka.			
		3. Kushughulikia matatizo ya wazalishaji ya bidhaa zinazosafirishwa nje.			
		4. Vyama vya wafanyabiashara kuwahamasisha wanachama wao kuanzisha kilimo cha biashara, uzalishaji kwa masoko ya nje, usindikaji na uchakataji wa mazao ya kilimo na usambazaji wa pembejeo.			

NGUZO YA 8 SAYANSI, TEKNOLOJIA NA RASILIMALI WATU KATIKA KUWEZESHA MAPINDUZI YA KILIMO					
	SHUGHULI	**MAJUKUMU**	**MKAKATI WA MKOA**	**MUDA WA UTEKELEZAJI**	**MTEKELEZAJI**
8.1	Kuanzisha utaratibu wa kutathmini matumizi yanayokidhi mahitaji ya kisayansi, kiteknolojia na rasilimali watu kwa ajili ya KILIMO KWANZA.	1. Kufuatilia na kutathmini wataalam wa kilimo waliopo.	Mkoa kuweka Kumbukumbu ya wataalam waliopo na Kuainisha mahitaji ya wataalam kwa kila kitengo katika ofisi ya Mkoa na Halmashauri.	Kuanzia 2010 Hadi 2015	Wakurugenzi Wa Halmashauri, Mkuu Wa Mkoa, Wakuu Wa Wilaya
		2. Kuwezesha maofisa ugani kuanzisha mashamba ya mfano na kuwapa wakulima maelekezo ya Kilimo bora.	Kufuatilia ili kuona kama Kila Halmashauri imetenga fedha katika mradi wa DADPS na kuanzisha mashamba ya mfano na mashamba darasa.		
		3. Kuweka malengo ya utendaji kwa maofisa ugani kama msingi wa tathmini ya ufanisi wao.	Kufuatilia ili kuona kama Kila Halmashauri imeandaa mpango kazi na kalenda ya kilimo kwenye eneo lake.Pia kuona kuwa wataalam wa ugani wameandaa mpango kazi na kalenda ya kilimo katika maeneo wanayosimamia.		
		4. Kuendesha Mafunzo ya 'Wakulima Wataalam' (Para Professionals) na kuwapeleka katika kila Kata.	Kuhakikisha kuwa wataalam wa Ugani wa Halmashauri wanatoa mafunzo kwa wakulima/wafugaji kutokana na mazao/mifugo wanayozalisha ,ambao watatumika kufundisha wakulima/ wafugaji wengine.	Kuanzia 2009	Wataalam Wa Kilimo/Mifugo

		5. Kuimarisha mafunzo kwa wataalam wa udongo na maji.	NA		
		6. Kuimarisha programu ya kuajiri wataalam wa kilimo wakiwemo wahandisi umwagiliaji, wataalam wa maji (hydrologists) wasanifu mabwawa, makandarasi n.k.	NA		

		7. Kuanzisha Bodi ya Usajili ya Wataalamu wa Kilimo	NA		
		8. Kuanzisha utoaji mikopo ya kilimo na ugawaji wa ardhi kwa wahitimu wa shahada ya Kilimo wenye sifa ya wajasiriamali.	NA		
		9. Kulipia mikopo ya gharama zote za masomo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu vya kilimo.	NA		
		10. Kutayarisha programu ya vivutio ili kuwavutia, kuwafundisha na kuwabakisha vijana katika kilimo.	NA		
		11. Kuingiza masuala ya jinsia katika KILIMO KWANZA na kuandaa programu za kuimarisha nafasi ya wanawake na vijana katika kilimo.			

		12. Kuanzisha vituo vya kutoa huduma na taarifa kama vile za pembejeo, matrekta ya kukodi na taarifa za masoko.	Kuhakikisha kuwa Kila Halmashauri inaanzisha na kuimarisha vituo vya utoaji taarifa (Resorce centres) katika maeneo yao.	Kuanzia 2010 Hadi 2015	Wakurugenzi Wa Halmashauri ,Mkuu Wa Mkoa, Wakuu Wa Wilaya
		13. Asasi za utafiti na mafunzo ya kilimo kutumia kwa ukamilifu sehemu ya mgao wa Serikali wa asilimia 1 ya pato la Taifa (GDP) kwa utafiti na maendeleo.	NA		
		14. Kuanzisha vituo vya hali ya hewa katika ngazi ya Kata.	Kuhakikisha kuwa Kila Halmashauri inaanzisha na kuimarisha vituo vya utoaji taarifa (Resorce centres) katika maeneo yao.		
		15. Kuanzisha utaratibu wa kuwa na vituo vya kuhifadhia taarifa mbalimbali za kilimo pamoja na masoko.		Kuanzia 2010 Hadi 2015	Wakurugenzi Wa Halmashauri ,Mkuu Wa Mkoa,Wakuu Wa Wilaya

NGUZO YA 9
UENDELEZAJI WA MIUNDOMBINU ILI KUWEZESHA MAPINDUZI YA KILIMO.

	SHUGHULI	MAJUKUMU	MKAKATI WA MKOA	MUDA WA UTEKELEZAJI	MTEKELEZAJI
9.1	Kubaini mahitaji ya uendelezaji miundombinu kwa ajili ya KILIMO KWANZA.	1. Kujenga miradi ya umwagiliaji ya kutosha kwa kulenga mazao ya kipaumbele, wingi wa mazao na mahitaji ya mahali pa uzalishaji.	Kupitia Miradi ya DADPS Mkoa utahakikisha kuwa mito iliyopo inatumika katika kilimo cha umwagiliaji wa mboga na matunda,Kuchimba visima virefu na vifupi na kuvuna maji ya mvua .	2010 hadi 2015	TAMISEMI, Wakurugenzi Wa Halmashauri
		2. Kuanzisha uwezo wa kutosha wa kuhifadhi mazao katika ngazi zote kwa mfano uhifadhi kwa majokofu, uhifadhi katika kaya, wilaya na taifa.	i.Kutoa elimu kwa wakulima /wafugaji juu ya uhifadhi wa mazao kama mboga ,matunda,maziwa,nyama,samaki na ngozi ii.Kuhamasisha Halmashauri ,kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali kujenga Masoko ya kisasa yenye miundombinu ya kuhifadhia mazao kama mboga,matunda,maziwa,nyama na samaki	2010 hadi 2015	Wakurugenzi wa Halmashauri Viongozi wa masoko
		3. Kutekeleza “Mpango Kabambe wa Mamlaka ya Bandari” (TPA Master Plan) unaojumuisha bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Mwambani na Bagamoyo. Vilevile bandari za Maziwa Makuu pamoja na bandari ya nchi kavu ya Kisarawe na uhamishaji wa mizigo baina ya Reli ya Kati na Tazara pale	NA		

		Kidatu.			
		4. Kukamilisha upanuzi wa uwanja wa ndege wa Mwanza ili uweze kutumiwa na ndege kubwa.	NA		
		5. Kukamilisha ujenzi wa viwanja vya ndege vya Mbeya, Iringa na vingine na kuwekeza vifaa vya kuhifadhi mazao ya bustani (maua, mboga na matunda) yanayosafirishwa nje ya nchi.	NA		
		6. Kukamilisha mtandao wa mkongo wa mawasiliano wa taifa na kuunganisha na mtandao wa chini ya bahari.	NA		
		7. Kuboresha mfumo wa reli na barabara	NA		
		8. Kujenga machinjio ya kisasa na viwanda vya kusindika nyama kila mkoa.	i.Kuhamasisha Halmashauri kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali na watu binafsi kujenga machinjio ya kisasa.	2010 Hadi 2015	Wakurugenzi Wa Halmashauri
9.2	Vituo vya Soko kwa kila Kata	Kuanzisha vituo vya soko katika ngazi ya Kata na kuviunganisha na vituo vya uzalishaji.	i. Kuhakikisha kuwa kila Halmashauri ya Manispaa inajenga vituo vya kukusanyia /kuuza mazao ambavyo vitaunganishwa na masoko mengine pamoja na wasindikaji.	2010 Hadi 2015	Wakurugenzi Wa Halmashauri
9.3	Kupeleka Umeme vijijini kwa ajili ya kuboresha Kilimo	Kutenga mtaji wa kutosha kwa ajili ya Mfuko wa Nishati Vijijini	NA		

NGUZO YA 10 UHAMASISHAJI NA USHIRIKISHWAJI WA WATANZANIA KUUNGA MKONO NA KUTEKELEZA KILIMO KWANZA					
	SHUGHULI	**MAJUKUMU**	**MKAKATI WA MKOA**	**MUDA WA UTEKELEZAJI**	**MTEKELEZAJI**
10.1	Kuingiza Kilimo KWANZA katika vyombo na mipango ya Serikali	Kuingiza KILIMO KWANZA katika mipango ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.	Kuhakikisha kuwa Mkoa na Halmashauri zinatoa kipaumbele katika kilimo wakati wa kupanga mipango ya maendeleo	Kuanzia 2010 Hadi 2015	Wakurugenzi Wa Halmashauri, Mkuu Wa Mkoa,Wakuu Wa Wilaya
10.2	Kufanya kampeni ya uhamasishaji KILIMO KWANZA katika ngazi ya taifa, mkoa, wilaya kata, na vijiji	1. Kuchapisha na kuzindua kitabu cha KILIMO KWANZA	NA		
		2. Kuhamasisha shule na vyuo kushiriki katika kampeni ya KILIMO KWANZA			
		3. Wabunge, Uongozi wa Mikoa na Wilaya kueneza taarifa zinazohusu KILIMO KWANZA.	Viongozi wa ngazi zote za Mkoa na wilaya kuhamasisha wakulima kwa kufanya kampeni za kilimo Kwanza. Mkoa kuweka Agenda ya Kilimo kwanza katika vikao vya kisheria mfano RCC.	Muda Wote	Viongozi Wote
10.3	Kuhamasisha Sekta Binafsi kushiriki katika KILIMO KWANZA	1. Kuimarisha ushiriki wa sekta Binafsi katika utekelezaji wa KILIMO KWANZA.	Kuhamasisha Ujenzi wa vituo vya kutoa taarifa kwa Wakulima.	Muda Wote	Wakurugenzi Wa Halmashauri, Mkuu Wa Mkoa,Wakuu Wa Wilaya
		2. Kushirikisha vyombo vya habari katika kutangaza KILIMO KWANZA			

10.4	Viongozi kushiriki katika kilimo.	Kuhamasisha viongozi katika ngazi zote kujihusisha binafsi katika uzalishaji chini ya KILIMO KWANZA			
10.5	Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa KILIMO KWANZA	Kutayarisha na kuchapisha taarifa za robo mwaka za maendeleo ya utekelezaji wa KILIMO KWANZA.	Kuhakikisha kuwa Kila Halmashauri inaandaa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Kilimo Kwanza na kuziwasilisha Mkoani kwa wakati uliokubalika.	Kuanzia 2009	Wakurugenzi wa Halmashauri